



“Je, nisiwaambieni matendo bora zaidi kwenu, na masafi zaidi mbele ya Mfalme wenu, na yatakayo kunyanyueni juu zaidi katika daraja zenu

Kutoka kwa Abuu Dardaa -Radhi za Allah ziwe juu yake- Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: “Je, nisiwaambieni matendo bora zaidi kwenu, na masafi zaidi mbele ya Mfalme wenu, na yatakayo kunyanyueni juu zaidi katika daraja zenu, na bora kwenu kuliko kutoa dhahabu na pesa, na bora kwenu kuliko hata kukutana na adui yenu na mkapiga shingo zao na wakapiga shingo zenu?” Wakasema: Ndiyo. Akasema: “Ni kumtaja Mwenyezi Mungu”.

[Sahihi] [Imepokelewa na Tirmidhiy, Ibn Majah na Ahmad]

Maswahaba walimuuliza Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Hivi je mnata nikuelezeni na nikufundisheni amali bora zaidi kuliko zote katika amali zenu, na yenye utukufu kuliko zote na yenye kukua zaidi na safi zaidi na takatifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu Mfalme Aliyetukuka? na yenye nafasi ya juu zaidi katika nafasi zenu za peponi? na ambayo ni bora zaidi kwenu kuliko kutoa sadaka ya Dhahabu na fedha? na bora kwenu kuliko hata kukutana na makafiri vitani, mkapiga shingo zao, na wakapiga shingo zenu? Maswahaba wakasema: Ndio tunalitaka hilo. Akasema rehema na amani ziwe juu yake: Ni kumtaja Mwenyezi Mungu katika nyakati zote na katika mikao yote na hali zote.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3575>

